

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI

10 MEI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA ISHIRINI NA MBILI – TAREHE 10 MEI, 2023

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA MAJI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

280. MHESHIMIWA ATHUMANI ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya mkato kutoka Kigwe B hadi Magiri Uyui ili kuchepusha magari makubwa kupita Tabora Mjini.

281. MHESHIMIWA MICHAEL MWITA KEMBAKI (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani kuondoa tatizo la Wanafunzi kusoma kwa zamu katika Halmashauri ya Mji Tarime.

282. MHESHIMIWA TARIMBA GULAM ABBAS (KINONDONI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itawaongezea TARURA bajeti ili barabara za ndani za Jimbo la Kinondoni zijengwe kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**283. MHESHIMIWA JOSEPHAT SINKAMBA
KANDEGE (KALAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Mahakama yenye hadhi ya Wilaya katika Wilaya ya Kalambo.

**WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA
BIASHARA:**

**284. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali imejipangaje kuwawezesha Wajasiriamali kwa kuwapatia ujuzi na mafunzo.

WIZARA YA MAJI:

**285. MHESHIMIWA GRACE VICTOR TENDEGA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itamaliza kujenga Mradi wa Maji katika Vijiji vya Sawala, Mtwango, Rufuna na Kibao vilivyopo Mufindi Kusini.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO
YA MAKAZI:**

**286. MHESHIMIWA SUMA IKENDA FYANDOMO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:-

Je, lini Serikali itapeleka Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya ya Rungwe.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**287. MHESHIMIWA LUHAGA JOELSON MPINA
(KISESA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, kwanini ilitumika njia ya *Single Source* kumpata Mkandarasi wa SGR LOT N 6 Tabora – Kigoma na kusababisha hasara ya Trilion 2.

288. MHESHIMIWA TASKA RESTITUTA MBOGO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mpanda hadi Karema kwa kiwango cha lami.

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:

289. MHESHIMIWA FLORENT LAURENT KYOMBO (NKENGE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itaongeza Minara na kuboresha Mawasiliano katika Kata zote 20 za Wilaya ya Misenyi.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

290. MHESHIMIWA MWATUM DAU HAJI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itaongeza gari la Polisi Wilaya ya Kusini Unguja kwa kuwa gari lililopo halikidhi mahitaji.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

291. MHESHIMIWA ERIC JAMES SHIGONGO (BUCHOSA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi VETA Buchosa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAJI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

**DODOMA
10 MEI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**